



Maswali na Majibu

1. Mbona Paulo alienda Dameski?
Alienda kuwashika na kuwatesa Wakristo.
2. Nini ilifanyika kwa Paulo njiani?
Yesu alizungumzia na akabadi.
3. Mbona wanafunzi walihubiri Injili kwa Wayahudi?
Kwa sababu ahadi za Mungu zilikuwa kwa Wayahudi, watu wake.
4. Mataifa wanakuwa kwa familia ya Mungu namna gani? Mungu alichagua nani kuhubiria Mataifa?
Kwa kubatizwa. Mungu alichagua Paulo.
5. Paulo alienda kuhubiri Injili na kusimamisha makanisa wapi?
Katika Milki ya Roma yote – Giriki, Asia (Turuki) na Italia.
6. Paulo alikuwa na ziara ngapi akienda kuhubiri Injili? *Ziara 3.*
7. Taja baadhi ya mateso yenye Paulo alipata kwa ziara zake.
Meli kufunjika, kufungwa gerezani, kupigwa viboko, kupigwa mawe, hatari njiani, baridi, njaa n.k.
8. Nini ilifanyika kwa Paulo Yerusalem?
Wayahudi walifanya ghasia, Paulo akashikwa. Akawa gerezani kwa miaka 2.
9. Mbona Paulo alienda Roma? Alifanya nini kule?
Alienda kuhukumia kwa haki na Kaisari. Alihubiri injili na kuandikia makanisa barua.
10. Nini iliwa ya maana kwa Paulo kuliko mateso aliyoyapata?
Upendo kwa Mungu, kwa Yesu na tumaini la wokovu.

Mistari ya kukariri

Wagalatia 3:27 – 29

Wafilipi 3:8

2 Timotheo 4:2

Mazungumzo

Baada ya Paulo kubadili, alitumia maisha yake kuhubiri Injili na alikuwa na mateso mengi. Mbona alifanya hivi? Lazima tuhubiri Injili. Tunajifunza nini kutoka kwa Paulo? Soma 1 Wakorintho 9:19 – 23.

Kuandika

Chagua moja ya hii miji na uandike yaliyompata Paulo kule:

Listra, Filipi, Korintho, Efeso, Troa, Melita

Masomo ya watoto wakubwa wa CBM

Somo la 41 Paulo Mtume wa Mataifa

SOMA Matendo 9:1 – 19; Wagalatia 3:26 – 29; 2 Wakorintho 11:24 – 27;
Matendo 14:8 – 15; 16:16 – 34; 18:1 – 4; 19:23 – 41; 20:7 – 12; 28:1 – 6

SOMO

Sauli alikuwa Mfarisayo. Alisomea sheria hapo Yerusalem. Sauli aliudhiwa sana na mafundisho ya Wakristo hapo Yerusalem. Sauli alichukia Wakristo. Alikataza watu wasifundishe juu ya Yesu. Sauli aliona Stefano akipigwa mawe. Alitesa Wakristo wengi sana na kuwatupa gerezani Yerusalem. Alisikia kwamba kuna Wakristo wengi sana Dameski. Alisafiri kwenda huko ili awatese na kuwashika Wakristo waliokuwa kule.

Sauli alipokaribia Dameski, kwa ghafula nuru ikamwangazia kote kote kutoka mbinguni. Alianguka chini na akasikia sauti ikimwambia, “Sauli, Sauli, mbona wanitesa?” Sauli aliuliza, “U nani wewe Bwana?” Bwana alijibu, “Mimi ndimi Yesu, unayenitesa. Inuka uingie mjini. Utaambwa cha kufanya.” Sauli alipofungua macho, alikuwa kipofu. Watu wake walimwongoza mpaka Dameski.

Yesu alituma Mkristo, Anania aende kuona Sauli. Yesu aliambia Anania kwamba alikuwa amemchagua Sauli kuhubiria Mataifa. Anania alimsaidia Sauli ili apate kuona tena. Alimpa Sauli kipawa cha Roho Mtakatifu. Papo hapo Sauli alibatizwa. Alibadilishwa na kuwa Mkristo. Sauli alibadilisha jina na kuitwa Paulo.

Yesu na wanafunzi walikuwa Wayahudi. Ahadi za Mungu kwa Ibrahimu na Daudi zilikuwa kwa watu wake, Wayahudi. Hapo awali Injili ilihubiriwa kwa Wayahudi pekee. Wayahudi walikuwa na shida kukubali kwamba Mataifa nao wanashirikishwa kwa ahadi za Mungu. Hawakuelewa kwamba Mungu alitaka mataifa yote yapate wokovu katika Yesu.

Soma Wagalatia 3:26 – 29. Wote wanaobatizwa ndani ya Yesu Kristo wanahuksiana kwa Kristo. Wanakuwa wamoja kwa familia ya Mungu. Watu wa Mataifa wanaobatizwa wanakubali kuwa Wayahudi na wanasehemu kwa ahadi za Mungu.

Zaidi wanafunzi walihubiria Wayahudi. Mungu alimchagua Paulo ahubirie Mataifa.

Kazi ya Paulo ilikuwa kueneza habari ya Yesu na Ufalme wa Mungu kwa nchi zingine katika Milki ya Warumi. Paulo alienda ziara tatu kubwa akihubiri Injili kwa Mataifa. Alihubiri Injili huko Asia (sasa inaitwa Uturuki), Giriki na Italia. Paulo alisimamisha kanisa ya Wakristo kwa Milki yote ya Roma.



Kawaida Paulo hakukuwa akisafiri peke yake. Kwa ziara yake ya kwanza alikuwa na Barnaba. Baadaye alisafiri na Timotheo, Luka, Sila na wengine. Hizi safari zilikuwa za pole pole na wakati mwininge za hatari. Safari zake nyingi zilikuwa za kwenda mbali na za bahari. Mara tatu meli zilikuwa zikifunjika. Siku mzima alikaa baharini usiku na mchana. Wakati mwininge alisafiri kwa barabara kubwa za Roma. Kwa hizo barabara kulikuwa na hatari na ugumu. Hata kulikuwa na wanyan'ganyi waliojificha kwa miamba.

Paulo alipowasili mji wowote, kwanza alihubiria Wayahudi kwa sinagogi. Kawaida Wayahudi hawakufurahia mafundsho yake. Kwa hivyo Paulo aliacha Wayahudi na kwenda kuhubiri Injili kwa waliotaka. Paulo alifundisha watu wengi Injili. Mara tu walipoamini, aliwabatiza. Paulo alifundisha waumini wapya vile wanatakiwa kuabudu Mungu na vile wanaweza kumega mkate, kukumbuka Yesu kama dhabihu. Paulo alisimamisha kanisa ya Wakristo karibu kwa kila mji alikozuru. Baada ya muda alienda mji mwininge.

Kwa ziara yake ya pili na ya tatu, Paulo alizuru kanisa nyingi zenyne alikuwa ameanzisha mapema. Aliwapa moyo na kuwasaidia. Pia Paulo aliandika barua kwa kanisa zenyne alikuwa amesimimsha. Hizi kanisa zilikuwa mpya sana. Walikuwa na maswali na shida. Paulo aliwaandikia barua za kuwapa moyo. Tuna baadhi ya hizi barua za Paulo kwa Agano Jipy.

Paulo alipitia kwa mambo mengi ya ujasiri na ikampa ufahamu mkuu kwa hizo ziara zake. Tafuta kwa ramani maeneo yenye Paulo alikuwa akipitia na ujue alichofanya kule.

| | |
|-----------------|--|
| Listra | Paulo aliponya kiwete. Watu walitaka kuwatolea Paulo na Barnaba dhabihu. Matendo 14:8-15. |
| Filipi | Paulo na Sila waliwekwa gerezani. Mungu alituma malaika akawafungua na wakawa huru. Matendo 16:16-34. |
| Korintho | Paulo alikutana na Akila na Prisila waliokuwa watengenezaji wa mahema kama yeye. Matendo 18:1-4. |
| Efeso | Wafua fedha walifanya ghasia kwa uwanja wa michezo kwa sababu Paulo alisema kwamba miungu yao si ya kweli. Matendo 19:23-41. |
| Troa | Eutiko alianguka kutoka kwa dirisha. Paulo alimfufua kutoka kwa wafu. Matendo 20:7-12. |
| Melita | Meli ya Paulo ilivunjika. Nyoka wa sumu alijifunga kwa mkono wake lakini hakuumizwa. Matendo 28:1-6 |

Watawala wa Wayahudi hawakupenda Wakristo. Walijaribu kuzuia Paulo asihubiri. Kila mara walimshambulia Paulo na kumweka kwa shida. Wakati mwingu walipanga kumuua. Paulo aliumia sana kwa sababu ya kuhubiri Injili. Soma chenye Paulo anasema kwa 2 Wakorintho 11:24-27.

Wayahudi walimchukia Paulo na wakapanga kumuua. Alipokuwa Yerusalem, Wayahudi walifanya ghasia halafu Paulo akashikwa na askari wa Kirumi. Paulo aliwekwa gerezani kwa zaidi ya miaka miwili. Baadaye Paulo aliuliza apelekwe Roma kwa Kaisari kwa hukumu ya haki. Alipelekwa Roma kwa meli.

Huko Roma Paulo aliishi kama mahabusi kwa nyumba ya kukodesha karibu miaka miwili. Alikuwa amefungwa kwa askari wa Roma. Paulo aliendelea kufanya Mungu kazi. Alihubiri Injili kwa kila mtu aliyeuja kumwona na akaandika barua nyingi sana kwa makanisa aliyokuwa amesimamisha.

Alihukumiwa kwa Kaisari. Labda hapo ndiyo aliua. Upendo kwa Mungu na kwa Yesu na tumaini ya wokovu vilikuwa vya maana zaidi kuliko mateso aliyopata. Yesu atakaporudi hapa duniani, atafufua Paulo kutoka kwa wafu. Paulo ataishi milele kwa Ufalme wa Mungu waajabu hapa duniani.